# POPATLAL SECONDARY SCHOOL

**P.O.BOX 5007 Tanga City, TANGA**
**TANZANIA**

Kwa Mzazi/Mlezi wa …………………………………………………………………………………….

## UTANGULIZI

Shule inayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao ……………………………………………………………. amechaguliwa kujiunga na Kidato cha ………………… kwa mwaka ………………..…. katika shule yetu. Mwanao anatakiwa kufika shule tarehe .............................. tayari kwa kuanza masomo akiwa na vitu vifuatavyo.

i. Nakala ya cheti cha kumaliza darasa la saba au barua kutoka kwa Mwalimu Mkuu wa shule aliyomaliza Darasa la Saba .

ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

iii. Picha nne (passport size)

**<u>ILANI:</u> Mzazi au Mlezi unaombwa kusoma kwa makini sheria na masharti ya shule kama yalivyoandikwa hapa**

1. **<u>ADA YA SHULE</u>**

Ada za shule ni kama zinavyo ainishwa hapa chini

| MCHANGANUO | KIASI |
|---|---|
| Ada, Stationary & Maabara<br>Transport<br>Chakula cha mchana | 1,000,000.00<br>500,000.00<br>500,000.00 |
| ***JUMLA*** | **2,000,000.00** |

2. **<u>GHARAMA ZA UNIFORM</u>**

Uniform zote za shule zitashoneshwa shuleni. Ni marufuku Mzazi/Mlezi kushonesha uniform nje ya shule. Kwa wasichana pair 2 gharama ni 150,000/= na kwa wavulana gharama ni 80,000/= kwa pair 2 (Uniform zimeainishwa kwenye kipengele cha 4.7 kwenye form hii). Pesa za uniform zilipwe kwenye Account ya Benki iliyoainishwa hapo chini, pamoja na shg. 25,000/= ya sweater kwa kila mwanafunzi.

**3. (a) <u>Jinsi ya kulipa ADA na malipo mengineyo:</u>**

Unatakiwa kulipa ada ya shule kupitia Benki ya:

I. **DIAMOND TRUST BANK (D.T.B)**

JINA LA AKAUNTI: **IBADHIY MUSLIM ASSOCIATION OF TANGA**

NAMBARI YA AKAUNTI: **0055724002**

Shule haitapokea fedha taslimu kutokana na sababu za kiusalama**. Kumbuka jina la mwanao lazima liandikwe kwenye "PAY SLIP" kwenye sehemu ya "DEPOSITED BY …………".** Kwa watakaofanya malipo kwa cheque, post dated cheque hazitoruhusiwa na risiti itatolewa baada ya cheque kupita (baada ya siku tatu za kazi).

**(b)MIKUPUO YA ULIPAJI ADA**

| **MIKUPUO** | **TAREHE** | **KIASI** |
|---|---|---|
| Mkupuo wa kwanza<br>Mkupuo wa pili<br>Mkupuo wa tatu<br>Mkupuo wa nne | 1 Desemba - 31Desemba<br>1 Machi - 31 Machi<br>1 Juni – 30 Juni<br>1 Sept – 15 Sept | 700,000.00<br>500,000.00<br>500,000.00<br>300,000.00 |
| **JUMLA** | | **2,000,000.00** |

Ikiwa mtoto atasimamishwa kutokana na makosa ya kinidhamu, atawajibika kulipiwa mkupuo wa kipindi husika kama hajalipiwa.

**I. <u>MITIHANI YA NJE</u>**

**Mzazi atawajibika kumlipia mtoto wake mapema ada za mitihani ya nje kama ifuatavyo: (MALIPO HAYA YAFANYIKE SHULENI NA SIO BANK))**

| **AINA YA MTIHANI** | **KIDATO** | **GHARAMA** |
|---|---|---|
| Mtihani wa mock<br>Mtihani wa Mock (Islamic)<br>Mtihani wa Taifa | II<br>II<br>II | 20,000.00<br>10,000.00<br><u>20,000.00</u> |
| | **JUMLA** | **<u>50,000.00</u>** |
| Mtihani wa Mock<br>Mtihani wa Mock Tanga (Islamic)<br>Mtihani wa Mock Taifa (Islamic)<br>Mtihani wa Taifa | IV<br>IV<br>IV<br>IV | 20,000.00<br>20,000.00<br>25,000.00<br><u>55,000.00</u> |
| | **JUMLA** | **<u>120,000.00</u>** |

**<u>NB:</u>** michango mingineyo kama kuwabakisha wanafunzi wa darasa la Mtihani wa Taifa kipindi cha likizo mzazi atafahamishwa kwa maandishi utaratibu wa jinsi ya kuchangia kwa ajili ya **chakula**, **malazi** na **kumkimu mwalimu**.

## SHERIA ZA SHULE:

### 3.1 Mahudhurio

- i Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni kwa kutumia usafiri wa shule.
- ii Ni marufuku mwanafunzi kuchelewa kuingia darasani au kuwahi kutoka darasani.
- iii Mwanafunzi atalazimika kuhudhuria vipindi vya ziada kama vitakavyo pendekezwa na uongozi wa shule au mwalimu wa somo.
- iv Mwanafunzi atakae kosa kuhudhuria shule kwa miezi mitatu (3) mfululizo bila taarifa atakuwa amejifukuzisha shule.
- v Mwanafunzi akiwa mgonjwa, mzazi atoe/alete taarifa shuleni au aje na cheti cha matibabu kuthibitisha, kinyume na hapo atarejeshwa nyumbani akamlete mzazi wake.
- vi Mwanafunzi hatoruhusiwa kutoka nje bila ya kibali maalum kilicho idhinishwa na Mkuu wa Shule .
- vii Endapo kuna dharura yeyote mzazi atoe taarifa **RASMI** kwa Mkuu wa Shule au mwalimu wa darasa na pia ampigie dereva mapema gari isiharibu mafuta kumfuata namba za simu zitatolewa shuleni.
- viii Ukaguzi wa mara kwa mara utafanyika kwa wanafunzi wote.
- ix Atakaebainika kuja na vitu vilivyopigwa marufuku atafukuzwa shule.
- x Mwanafunzi haruhusiwi kugusa kamera (CCTV) au kucheza jirani na zilipo kamera (CCTV) katika maeneo yote ya shule.

### 3.2 Lugha:

Lugha rasmi ya mawasiliano, kufundisha na kujifunzia darasani na nje ya darasa lazima iwe ***KINGEREZA***, adhabu itatolewa kwa anaye kiuka amri hii. Aidha kwa masomo ya Kiswahili, Kiarabu na elimu ya dini ya kiislamu yatafundishwa kwa lugha husika.

### 3.3 Taaluma :

Lengo la shule ni kuwaandaa wanafunzi wapate ufaulu wa juu katika mitihani yao na kuleta ushindani katika ngazi ya Taifa. Ili kufikia malengo haya mwanafunzi anatakiwa azingatie yafuatayo:-

a. Mwanafunzi atumie muda wake kikamilifu katika masomo na wazazi watoe ushirikiano wao kwa watoto wao.

b. **Mwanafunzi azingatie nidhamu za darasani kama zifuatavyo .**

   - i. Kutopiga kelele.
   - ii. Kufuatilia kwa makini masomo yanayo fundishwa bila kuhangaika.
   - iii. Kufanya kazi zote za darasani kwa wakati uliopangwa bila kuchelewa au kutoa kisingizio chochote.
   - iv. Kutosinzia darasani .
   - v. Kutofanya jambo lolote lisilohusiana na somo linalo endelea
   - vi. Hairuhusiwi kula, kutafuna au kunywa kitu chochote darasani
   - vii. Mwanafunzi anatakiwa kunakili 'notes' zote zinazo tolewa na kufanya masahihisho ya kazi alizo zikosea chini ya usimamizi wa mwalimu wa somo.
   - viii. Ni marufuku mwanafunzi kuzunguka zunguka au kusimama darasani bila sababu ya msingi.
   - ix. Akae kwenye sehemu yake ya kiti na meza kwa mkao wa kawaida.

c. Mwanafunzi atakaekosa kufanya jaribio lolote au mtihani kwa sababu za msingi **anatakiwa** amuone mwalimu wa somo husika apewe mbadala vinginevyo atapewa alama sifuri (zero).

d. **<u>Wastani wa ufaulu mwisho wa mwaka ni alama 65%.</u>** Mwanafunzi asipofikia wastani wa alama 65% katika mjumuisho wa majaribio na mitihani yake yote ya mwaka mzima (hata endelea) na darasa jingine hapa shuleni.

e. Kila mzazi ana haki ya kutumiwa matokeo ya maendeleo ya mtoto wake ya kila jaribio na mtihani na punde mzazi anapopata matokeo hayo atoe maoni yake na yatumwe au yaletwe shuleni katika tarehe iliyotajwa.

f. Mwanafunzi anatakiwa kuja na daftari za masomo (counter book) kumi na nne (14) pamoja na vifaa vingine vya darasani.

g. Lazima kila mwanafunzi awe na seti ya vifaa ya hisabati (mathematical set) na box file moja kwa kuhifadhia mitihani na majaribio yake.

h. Mzazi atalazimika kulipa gharama za ziada kwa mwanafunzi yeyote atakayekuwa chini ya wastani wa shule ili asomeshwe wakati wa likizo.

### 3.4 <u>Nidhamu:</u>

Shule yetu inazingatia maadili ya kiislamu, hivyo basi mwanafunzi anaejiunga na shule hii anatakiwa atekeleze yafuatayo:-

i Ni lazima mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wasiokuwa walimu, walimu na wanafunzi wenzake.

ii ***NI MARUFUKU mwanafunzi kuwa na mawasiliano au mahusiano ya aina yeyote ile ndani na nje ya shule kati ya mvulana na msichana. <u>Kosa la kuvunja amri hii adhabu ni kufukuzwa shule moja kwa moja .</u>***

iii Mwanafunzi haruhusiwi kwa namna yoyote ile na kwa mtu yeyote kutumia lugha chafu, kuchonganisha, kudhalilisha au kutania.

iv Mwalimu au mgeni anapoingia darasani/mahali popote mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kumpokea.

v Mwanafunzi anapojiunga na shule hii hatoruhusiwa kutumia mitandao ya kijamii akiwa ndani na nje ya shule kama **facebook, whatsapp, twitter,viber,tango,my people,instagram, n.k.**

vi Vifaa vyote vya electronics kama **simu, line, mp3, iPod, camera, radio nk. haviruhusiwi katika mazingira ya shule, mwanafunzi atakae kutwa navyo shuleni vitachukuliwa na havitorejeshwa pamoja na kufukuzwa shule** .

vii Ni marufuku nje na ndani ya shule kwa mwanafunzi **kuvuta sigara, bangi, kula mirungi, madawa ya kulevya, kunywa pombe, kutumia ugoro, pariki na vingine kama hivyo.**

viii Ni marufuku kupigana.

ix Ni marufuku mwanafunzi kushiriki tendo lolote la wizi.

x Wanafunzi wataruhusiwa **kutumia simu ya Mkuu wa Shule, kwa dharura ya kuwasiliana na wazazi wao tu**.

xi Wanafunzi wanatakiwa kudumisha nidhamu katika matumizi ya mali za shule mfano matumizi ya mafeni na kutoacha wazi mabomba ya maji.

xii Ni marufuku kwa mwanafunzi kuletewa au kuagiza chakula kutoka nje ya shule.

xiii Ni marufuku kwa wanafunzi wa jinsia tofauti kuchanganyikana kwa vyovyote vile wawapo katika eneo la shule. Adhabu yake ni kufukuzwa shule.

### 3.5 Ibada:

- Mwanafunzi wa kiislamu anawajibika kusimamisha swala zote tano ndani na nje ya shule. Kutokusimamisha swala kwa wanafunzi wa kiislam adhabu yake ni kufukuzwa shule.
- Wanafunzi watatakiwa kuwa na utulivu wa hali ya juu wanapokuwapo katika nyumba za ibada. Adhabu itatolewa kwa watakaoleta zogo na vurugu katika nyumba za ibada .
- Mwanafunzi wa kiislamu hatoruhusiwa kula ndani ya mwezi wa Ramadhani ila kwa dharura ya kisheria.
- Kufuata na kutii sheria za msikitini (sehemu maalum iliyoandaliwa kwa kufanya ibada) kikamilifu. Mwanafunzi atakaebainika kuvunja sheria za msikitini atapewa adhabu stahiki.

### 3.6 Utunzaji wa vifaa vya shule :

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza vifaa vyote vya shule anavyokabidhiwa au anavyoazimwa. Ni marufuku kuandika au kuchora vitabu (text books), kuta, mbao, madawati na viti. Mwanafunzi akipoteza au kuharibu kifaa cha shule kwa kukusudia au kwa uzembe, mzazi atalazimika kulipa pesa.

### 3.7 SARE ZA SHULE NA USAFI:

#### A. SARE ZA WAVULANA (DARASANI)

- Suruali mbili pana za kitambaa cha rangi ya kijivu (grey) bila marinda
- shati mbili za mikono mifupi
- Mkanda mweusi wa ngozi
- Jozi mbili za viatu vya ngozi nyeusi vya kufunga kwa kamba
- Jozi mbili za soksi nyeusi
- Beji za shule mbili zitakazoshonewa kwenye mfuko wa shati
- Flana mbili nyeupe za ndani (vest)
- Begi la shule la vitabu

**B. SARE ZA WASICHANA (DARASANI)**

- Juba la pink linalo vuka kiuno
- Jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga kwa kamba na visiwe na visigino virefu au mapambo
- Jozi mbili za soksi nyeusi
- Beji za shule mbili zitakazoshonewa kwenye blauzi
- Begi la shule la vitabu
- Wanafunzi wote watavaa Suruali mbili pana za kitambaa rangi ya kijivu (grey) na Baibui rangi ya kijivu (grey) badala ya short kanzu.

**ANGALIZO:**

i. Suruali kwa wasichana na wavulana zisiwe za kubana (vimodo) zikiwa zimebana atarudishwa nyumbani .
ii. Shati kwa wavulana ziwe pana na ndefu kiasi cha kuvuka mwisho wa zipu ya suruali.
iii. Wavulana wanatakiwa kuwa na nywele fupi zisizo nyolewa kimtindo, mfano pank, vipara,moohok n.k(wavulana wanatakiwa kunyoa namba moja au ½ cm).
iv. Ndevu na kofia sio sehemu ya sare ya shule.
v. Mapambo ya aina yeyote hayaruhusiwi kama hereni, bangili, mkufu, pete, hina, wanja, piko, kunyoa nyusi, kupakarangi mdomoni (lip shine), kikuku, rangi za kucha, mabanio ya nywele makubwa hayaruhusiwi.
vi. Wanafunzi wa kike wanatakiwa kufunga nywele zao kwa kitambaa cheupe cha ndani mabanio makubwa ya rangi hayataruhusiwa shuleni. Msichana atakaedhihirisha nywele zake atapewa adhabu kali.

**NB:**

- Kila mwanafunzi anatakiwa kuhakikisha kuwa sare imepigwa pasi na mwili wake ni safi na nadhifu kila siku.
- Hairuhusiwi mwanafunzi kufuga kucha,nywele au sharubu
- Karatasi, chupa tupu na uchafu wa aina yeyote uwekwe kwenye pipa la taka atake kaidi amri hii adhabu itatolewa.

### 4.0 Adhabu

Adhabu juu ya makosa zitakuwa zinatofuautiana kutokana na uzito na urudiaji wa makosa. Kama ifuatavyo:-

- Onyo la mdomo au nasaha
- Viboko
- Kusimamishwa masomo kwa muda
- Kufukuzwa shule

**5.0 <u>Makosa yanayo muachisha shule mwanafunzi</u>**

i. Wizi.
ii. Ulevi wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na madawa ya kulevya, kunywa pombe, kuvuta sigara, bangi, ugoro, pariki na mengineyo katika hayo.
iii. Makosa ya jinai.
iv. Kuharibu kwa makusudio mali binafsi/za umma na za wengine.
v. Kudharau bendera ya Taifa/ viongozi wa Serikali.
vi. Kuolewa.
vii. Kupata mimba
viii. Kutoa mimba au kushawishi au kushiriki kutoa mimba.
ix. Kushindwa kuhudhuria masomo darasani kwa siku 90 au zaidi.
x. Matumizi ya lugha chafu ya matusi.
xi. Kugoma, kuchochea pamoja na kushinikiza mgomo au kuonesha dalili yoyote ya kugoma.
xii. Kukataa adhabu halali kufuatia kosa la kukiuka sheria na taratibu za shule.
xiii. Kupiga au kupigana na mwanafunzi mwenzake au mfanyakazi wa shule.
xiv. Kumiliki simu au kufanya mawasiliano kwa njia ya simu kwa namna yoyote ile kinyume na utaratibu.
xv. Kutumia redio au vibawi vya muziki vya masikioni (headphone tape) anapokuwa shuleni.
xvi. Mwanafunzi atakaeharibu kamera (CCTV) ikithibitika, atalipia na kufukuzwa shule.
xvii. Kula njama ya kumnyima raha mwanafunzi au wanafuzni wengine na kuwakosesha amani na utulivu wanapokuwa hapa shuleni. Hii ni pamoja na uonevu na kutumia vitish

**<u>10 .HITIMISHO :</u>**

(REJESHA FOMU YA UKURASA WA 08 NA 09 OFISINI IKIWA IMEJAZWA) **Ndugu mzazi/mlezi, baada ya kusoma sheria hizi na kuzielewa tunaamini utashirikiana nasi katika kumfanya mtoto wako azielewe na kuzifuata sheria hizi, hivyo kufanikisha jukumu zito la kumlea mwano awapo hapa shuleni kitaaluma na kimaadili mema. Tunatarajia ushirikiano wako mkubwa.**

**<u>KUKIRI: UTHIBITISHO WA KUKUBALIANA NA MASHARTI YA SHULE</u>**

**Mimi mzazi wa ………………………………………………………… nakiri kusoma kwa makini kukubaliana na masharti yote ya shule. Ninachukua kikamilifu dhamana ya mtoto wangu ikiwa atakiuka au kujihusisha kuvunja sheria zilizowekwa na shule.**

**JINA LA MZAZI/ MLEZI: …………………………………………………**

**SAHIHI: ………………………………………………………………………**

**TAREHE: ……………………………………………………………………..**

***Bandika picha Kwa gundi***

**JINA LA MZAZI/MLEZI (1)……………………………………………………**

**SAHIHI…………………………………**

**TAREHE………………………………..**

**SIMU……………………………………**

***Bandika picha***
***Kwa gundi***

**JINA LA MZAZI/MLEZI (2)…………………………………………………………**

**SAHIHI…………………………….**

**TAREHE……………………………**

**SIMU………………………………….**

***Bandika picha***
***Kwa gundi***

**JINA LA MZAZI/MLEZI (3)……………………………………………………**

**SAHIHI…………………………………..**

**TAREHE………………………………..**

**SIMU………………………….**

***Bandika picha***
***Kwa gundi***

**NB: Tofauti na hawa wenye Picha hapa juu hakuna atakaeruhusiwa kumuona mwanafunzi.**
**Fomu ya hitimisho na cheti cha daktari virejeshwe shuleni.**

POPATLAL SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 5007, TANGA.

# MEDICAL CERTIFICATE

STUDENTS NAME: ____________________________________________________________

(To be completed by medical officer in charge)
I have examined the above named and consider that she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time education course.

(a) Eye sight ……………………………………………………………………………………………………

(b) Limbs ……………………………………………………………………………………………………

(c) Hearing ……………………………………………………………………………………………………

(d) Speech ……………………………………………………………………………………………………

STDS ……………………………………………………………………………………………………

(e) Leprosy ……………………………………………………………………………………………………

(f) Epilepsy ……………………………………………………………………………………………………

(g) Neuroses……………………………………………………………………………………………………

(i) Pregnancy ……………………………………………………………………………………………………

(j) Other serious diseases ……………………………………………………………………………

NAME: ……………………………………………………………………………………………………

SIGNATURE ……………………………………………………………………………………………………

STAMP ……………………………………………………………………………………………………

**TO THE HEADMASTER**
**POPATLAL SECONDARY SCHOOL**
**P. O. Box 5007, Tanga, City, TANGA**
**TANZANIA**